ILE MBEGU HAITARITHI PAMOJA NA KAPI

Na tuendelee kusimama kwa muda mdogo wa maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu.

2 Mungu mpendwa, twaona haya kuwa ni majaliwa makubwa usiku wa leo kuwa hapa wakati huu kuuletea Kristo, aliye hai ulimwengu unaokufa pamoja na kizazi kinachokufa.

3 Tungeuliza, Bwana, ya kwamba uyapake mafuta maneno yetu na juhudi zetu, ili yasikurudie bure, bali yatekeleze jambo ambalo yalikusudiwa.

4 Msaidie kila mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana hapa usiku wa leo aliye mhitaji. Na Baba, tunajua ya kwamba sote ni wahitaji. Na tunapoondoka usiku wa leo, na tujisikie mioyoni mwetu kama wale waliotoka Emau baada ya—wakiisha kushuhudia kufufuka kwa Kristo, wakisema, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Tujalie hayo, Bwana!

5 Waponye walio wagonjwa na wanaoteseka. Na asiweko ye yote mdhaifu miongoni mwetu baada ya ibada hii usiku wa leo. Na zaidi ya mambo yote, na kusiwe hata siyeamini mmoja aliyesalia, Bwana. Na wote waamini hadi Uzima wa Milele. Kwa sababu hilo ndilo kusudi la kukusanyika kwetu hapa.

6 Twaomba baraka hizi kwa ajili ya utukufu wa Ufalme wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina. (Mwaweza kuketi.)

7 Ni vizuri usiku huu kurudi hapa. Nami naona tuna watu wachache waliosimama huku, na nafikiri si—simu zimefunguliwa ku—kuelekea miji mingi mbali mbali nchini kote, San Francisco, Tucson, kule mashariki. Nasi kwa simu tunawatumia salamu. Tuko kwenye jumba la hotuba hapa usiku wa leo. Na jumba lenyewe limejaa kweli kweli, na marefu yake, na kote ukutani, kumejaa watu waliosimama. Na tunasikia ya kwamba kesho usiku tutajaribu kufungua upande mwingine hapa wa jumba hili la michezo ya viungo vya mwili kusudi tupate ukumbi mkubwa zaidi utakaochukua, labda, watu wengine elfu kadha. Kwa hivyo tunatarajia hayo kesho usiku. Iwapo imejaa kabisa usiku wa leo, usiku wa kwanza, naam, tunaamini itakuwa zaidi kesho usiku. Nami naona ya kwamba wameongeza viti vingine zaidi na kadhalika usiku huu.

8 Tunatazamia mambo makuu, kwanza...kule kuja kwa Bwana Yesu, halafu, wokovu wa—wa nafsi waliopotea ambao

watampokea usiku wa leo na wawe tayari kwa kuja Kwake atakapotokea.

9 Nataka kuwapa salamu maalum na kuwakaribisha watu hawa wazuri walio jukwaani ambao nafahamu wengi wao ni wahudumu. Mamia kadhaa au zaidi wameketi kwenye jukwaa, nasi bila shaka tunafurahia ya kwamba wako hapa.

10 Kwenu nyote watu po pote mlipo sehemu mbali mbali nchini. . . Nami nafahamu ya kwamba wengine wako hapa waliovuka bahari, nchi za ng'ambo. Kwa hivyo tuna shukrani kwenu kuwa hapa mkafurahie ushirika huu pamoja nasi, ambao tunatarajia Mungu atatupa katika mkutano huu.

11 Inaonekana kama kwamba tangu nilipofikiria kurudi huku kwa ajili ya siku hizi chache za mikutano, ya kwamba moyo wangu mwenyewe umeshtushwa ajabu na kujisikia sana ya kwamba jambo fulani liko karibu tu kutendeka. Sijui ni nini hasa, bali natumaini ya kwamba ni ufunuo mkuu kutoka kwa Mungu ambao uta—utatutayarisha na kutufanya raia bora zaidi wa Ufalme Wake tunapotembea katika ulimwengu huu wa giza na dhambi na kutokuamini.

12 Uwanja huu usiku wa leo, mahali papa hapa, pana jambo kubwa sana kwangu. Tangu nilipojua ya kwamba wamejenga jengo hili la shule hapa, nimetaka kufanyia ibada mahali hapa. Ninaishukuru sana halmashauri ya shule pamoja na wale walioturuhusu kwa hisani yao kuitumia. Ilikuwa mahali papa hapa hasa, yapata mahali fulani hapa jengo hili linaposimama usiku wa leo, ambapo jambo muhimu sana lilitokea yapata miaka thelathini iliyopita, papa hapa kwenye jengo lili hili. Hakukuwa kitu ila mbuga wakati huo. Nami naliishi katika kijumba kimoja ng'ambo kule, yapata yadi mia mbili. Nilihusika sana siku hizo na wokovu wa baba na mama yangu, ambao wote wawili wamekwisha kuaga dunia usiku wa leo. Na zaidi sana siku hiyo nilijishughulisha sana juu ya baba yangu.

13 Nakumbuka, nilikuwa nikilala ukumbini. Ilikuwa joto, majira ya kiangazi. Hii imeandikwa naamini kwenye kitabu kidogo kiitwacho, *Yesu Kristo, Yeye Yule Jana, Leo, na Hata Milele*, ama ilikuwa kwenye kijitabu kiitwacho, *"Sikuliasi Lile Ono la Mbinguni."*

14 Na nilipokuwa nimelala ukumbini, mara nikaamshwa, nami nikalemewa sana moyoni mwangu kwa ajili ya Baba yangu. Kama wengi wenu mjini humu mlivyomjua babangu, nafikiri alikuwa mtu mkuu, ingawaje alikuwa mwenye dhambi, na . . . lakini alikuwa na tabia baya ambayo nilijaribu kukomesha kitu hicho sana nilivyoweza wakati wote; hiyo ni kunywa pombe. Na usiku huo alikuwa akinywa. Nami nikaamka nimelemewa sana moyoni kwa ajili yake. Huku nikiwa na nguo za kulala tu, nikavaa suruari na kuacha shati la kulala, nikaondoka na

kuzurura humu mbugani ambapo jengo hili linasimama sasa. Nami nikapiga magoti kumwombea baba yangu.

15 Na nilipokuwa nikiomba na kumsihi Mungu amwokoe na asi—asimwachilie afe mwenye dhambi, ya kwamba nalimpenda . . . Na nilipokuwa nikiomba, nikainuka kutazama upande wa mashariki kutoka hapa, na ono likatokea. Na huku amesimama mbele yangu karibu sana nami (wengi wenu mnajua ono lile) alikuwa Bwana Yesu.

16 Naam, mimi si mwepesi wa kupata mazingaombwe kama nijuavyo; mbali maono ni dhahiri. Na hapo alisimama Bwana Yesu, mara ya kwanza nilipopata kumwona katika ono la namna hiyo. Alikuwa tu yapata, lo, futi kumi juu ya kichwa changu, amesimama hewani huku mguu mmoja ukipiga hatua. Alikuwa amevalia joho jeupe lenye tarizi ukingoni mwake. Nywele Zake zimening'inia mabegani Mwake, na alionekana ana yapata—mtu yapata jinsi Biblia ilisema alikuwa, yapata miaka thelathini, bali mtu mdogo, mwembamba, mdogo sana. Ilionekana kana kwamba hangalikuwa mwenye uzito wa ratili mia moja na thelathini.

17 Nami nikatazama, nikadhani huenda ikawa mna jambo ambalo huenda—nimekosea. Kwa hivyo nika—nikapangusa macho yangu na—na kutazama juu tena. Naye alikuwa amesimama kwa upande, umbo la uso Wake. Na kuonekana kwa uso Wake, ambao nimeuona daima katika maono, unafanana na picha ya kichwa cha Kristo katika umri wa miaka thelathini kilichochorwa na Hoffman. Hiyo ndiyo sababu ninayo nyumbani mwangu, vitabuni mwangu, po pote niwezapo kuiweka hiyo, kwa maana hivyo ndivyo ilivyokuwa, zinafanana sana. Isipokuwa alionekana mdogo.

18 Nami . . . Nilipokuwa nikimtazama, nikawaza, hakika simwangalii Bwana wangu akisimama pale. Nami nilikuwa, ningesema, mahali hivi, na huenda papa hapa ambapo hii—chini ya ilipo mimbara hii sasa. Mahali fulani, ilikuwa mumu humu karibu katikati ya eneo la mzunguko, toka mahali hapa ninaposimama, vyema niwezavyo kupima, ni kati ya yadi arobaini au hamsini, mahali fulani kwenye mviringo huu hapa.

19 Nikainua macho yangu, Naye alikuwa amesimama pale. Nami nikauma kidole changu kuona kama nilikuwa nimelala, unajua jinsi una . . . inaonekana tu kama kwamba sivyo. Nami nilikuwa tu mtu mchanga katika Bwana wakati huo, nilikuwa nimehubiri yapata miezi sita. Nikauma kidole changu. Nikachukua unyasi na kuuvunja. Baadhi yenu watu mnaoishi hapa nchini, mnajua jinsi kile kijiti cha kuchokoa meno cha zile nyasi kilivyo. Nikaanza kukitafuna. Nami nikasema. "Hai—haiwezekani. Mimi ninaota. Nyumbani kwetu ndiko kule. Baba, mama na watoto wako kule. Na pale kulikuwa kile kidimbwi cha kile kilichoitwa nyumba ya matofali kule chini, nilimokuwa

nikiwinda bata karibu yadi mia mbili kutoka hapa. Nami nimesimama mbugani; haina budi kuwa hivyo."

20 Nikapiga ardhi teke, nikakanyaga kwa miguu yangu kwa nguvu kidogo, na kutikisa kichwa changu na—na kusugua-sugua mikono yangu, kainua macho yangu tena, na kuangalia upande mwingine, katazama tena; Ndiye huyo amesimama pale. Na upepo ukaanza kuvuma, nami nikaona zile nyasi zikipeperushwa. Na zilipoanza kupeperuka, mavazi Yake yakapeperuka nazo. Kama nguo zilizoanikwa kwenye kamba, yakaanza ku—kupeperushwa.

21 Alikuwa amesimama pale. Nikamtazama. Nami nikawaza, "Laiti ningaliutazama uso Wake." Naye alikuwa akitazama upande wa mashariki, vivi hivi. Alikuwa akichungulia sana. Nami nikapiga hatua moja mbele nipate kuutazama uso Wake vizuri zaidi, ingawaje singeweza kumwona vizuri sana. Na mikono Yake mbele Yake, imefichwa kutoka mahali niliposimama.

22 Nami nikasongea tena, nikajikohoza hivi; nikafanya [Ndugu Branham anaonyesha—Mh.] kuona kama ningalimtazamisha. Bali hakujimudu.

23 Ndipo nikawaza, "Labda nitamwita." Niliposema, "Yesu," akageuza kichwa Chake; na aliponitazama, aliinua tu mikono Yake. Hilo tu ndilo ninalokumbuka kwa karibu. . .Karibu mchana kutwa nilikuwa nimelala papa hapa mahali fulani hapa uwanjani mjengo huu uliko, shati langu la kulala limelowa machozi ambapo nilikuwa nikilia, nami nikazimia. Uso Wake ulikuwa na sura ambayo hakuna mchoraji anga—angaliweza kuchora ama kutia rangi. Hawangaliweza kufanya hivyo. Alionekana kama Mtu ambaye kama ungalimtazama, ungelitaka kulia kwa kumhurumia na kumheshimu kwa kicho, walakini mwenye uweza wa kutosha hivi kwamba kama angalinena ulimwengu ungalipinduka. Na hiyo sura haingalichorwa na mchoraji.

24 Nami sikujua hata wa leo maana yake. Bali ndimi huyu usiku wa leo baada ya miaka thelelathini nimesimama kwenye jumba la hotuba lililowekwa wakfu sasa kwa ajili ya utumishi wa Mwenyezi Mungu. Nami ni mtu tu—mfuasi, hasa m—mzee wa mahali hapa katika—katika kanisa la Kibatisti hapa, ambapo Roy Davis alikuwa mchungaji wakati huo. Nami sasa ninasimama hapa huku mahali hapa pamejaa watu, mahali pale pale pamoja na—ninavyofikiria, ni walionunuliwa kwa Damu ya Yesu Kristo Mwenyewe mikononi mwangu kuleta ujumbe huu wa Bwana katika muda wa siku nne.

25 Yapata karibu miezi sita baadaye nilikuwa na ubatizo wangu wa kwanza chini hapa mtoni wakati ile Nuru iliposhuka papa hapa Spring Street, wengi wenu huenda mngetaka kwenda huko chini, mkaitazame, kule Spring Street and Water, papo

hapo ukingoni mwa mto. Na hapo ndipo Malaika wa Bwana alipojitokeza kwa watu hadharani kwa mara ya kwanza, na—saa 8 alasiri moja. Na sauti ikatoka Kwake, kasema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia kuja kwa pili."

26 Hii ni miaka thelathini baadaye, na ndimi huyu usiku wa leo ningali nikiutangaza Ujumbe huo. Na umezunguka dunia nzima, nami nafurahia kurudi katika mji wa nyumbani mwangu usiku wa leo kumwakilisha huyu Bwana Yesu Kristo ambaye ningali nampenda kwa moyo wangu wote. Kila siku Yeye anakuwa mtamu zaidi kuliko alivyokuwa siku iliyotangulia. Mimi sijabadilisha hata nukta moja ya mafundisho yangu. Jambo la kwanza nililoanza nalo, ningali naamini jambo lile lile usiku wa leo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

27 Sasa, nina Ujumbe fulani ambao ni jukumu langu. Ujumbe huu ulipoanza, bila shaka ulikuwa...Kila mtu alikuwa akiwaombea wagojwa, ishara kuu, maajabu, na miujiza, iliyoanza hasa katika watu wa Kipentekoste, ufufuo wa dunia nzima wa mikutano ya uponyaji ulioenea ulimwenguni. Kwa muda wa miaka kumi na mitano iliyopita kumekuwa na ufufuo kwenye kila kilima kilichoko, nakisia. Mioto ya ufufuo inawaka. Mamilioni wamemkubali Kristo kama Mwokozi wao kwa agizo hilo moja. Hilo limewatia moyo watu kama Oral Roberts, na kadhalika, na kote kote kila mahali, baada ya kanisa la Kipentekoste kulala uzingizi mzito kama ilivyokuwa wakati huo.

28 Nia yangu na hamu yangu usiku wa leo ni kuliamsha kanisa hilo tena kwa ajili ya kule kuja kwa Bwana Yesu kunakokaribia. Sina budi kulikemea. Sina budi kukemea dhambi ya kila namna. Siyaelekezi kwa dhehebu la mtu ye yote. Nina Ujumbe.

29 Naam, ni vigumu kuliendea kanisa nikadhaminiwe kama tu ilivyokuwa kwa Bwana wetu Yesu; maana ni Yeye; si mimi. Bali kama alivyohubiri hapo mwanzo, na kuwaponya wagonjwa, kawafufua wafu, na kuwatakasa wenye ukoma, na kutoa pepo, kila mtu alimtaka Yeye. Bali inafikia wakati ambapo mna Ujumbe ambao kila mara hufuatana na kila ishara, kwa maana ishara ina sauti. Bali alipoketi siku moja na kusema, "Mimi na Baba tu Mmoja!" hawangestahimili hilo.

30 Vivyo hivyo aliposema, "Msipoula mwili Wake Mwana wa Adamu na kuinywa Damu Yake, hamna uzima ndani yenu."

31 Inge...Naam, madaktari na watu wenye akili timamu wangalisema, "Mtu huyu ni kizuu kifyonza damu, anajaribu kuwafanya mle mwili wake ni kunywa damu yake." Yeye hakueleza hilo kamwe; alisema tu hivyo.

32 Na usiku wa leo huenda ukasikia mambo na kote mkutanoni ambayo yanasemwa, huenda tusiweze kuyaeleza, bali kumbuka, Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunaamini hilo!

33 Naam, hatuna muda wa kunena sana, kwa sababu tuna wakati fulani wa kuanza hapa na wakati fulani wa kutoka. Nasi tunataka kuheshimu halmashuri ya shule iliyoweka nyakati hizi kwa ajili yetu. Nasi tutafanya tuwezavyo kuwaheshimu.

34 Kumbukeni, wakati wo wote mwenye dhambi anapotaka kumjia Kristo, yote ikupasavyo kufanya ni kuja moja kwa moja humu hata ikiwa ninahubiri, kuimba, cho chote kile, na kutoa uhai wako kwa Kristo papo hapo na kusimama kitini mwako. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa, kukusaidia.

35 Nataka kuzungumza na Ndugu Vayle, Ndugu Borders, na wandugu hapa. Kama. . .Nashangaa kama alasiri ya leo kanisani, ama asubuhi yo yote, au cho chote kile, wangekuwa na ibada ya mafunzo kwa wale wanaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu? Hiyo ingekuwa sawa, ninyi wandugu, Ndugu Neville na ninyi nyote mngekuja hapa, Ndugu Capps?

36 Kama ye yote angetaka kushauriwa katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, mbona usije maskanini [Ndugu Branham anauliza saa—Mh.] yapata saa 4:00 asubuhi.

37 Kama una swali kuhusu haya mafundisho, kama una swali kuhusu Ujumbe huu, iwapo—iwapo unataka ku. . .Kama haujahudumiwa kibinafsi kamwe, unataka kuombewa, ama cho chote unachotaka kujua na watu hao. . .Mbona usijipenyeze tu kule chini saa 4:00 asubuhi ukawaone watu hawa. Kutakuweko mmoja au wengi wao pale kukushauri, kuombea wagonjwa, kujibu maswali jinsi tu mtu binafsi angalifanya. . . Wa—waendee tu nao watafurahia kukusaidia kwa njia yo yote wawezayo.

38 Sasa, kabla tu hatujaliendea Neno, tunataka kumwendea Mwandishi wa Neno tena. Huenda ukala kupita kiasi; huenda ukanywa kupita kiasi; huenda ukacheka kupita kiasi, huenda ukatembea sana; bali huwezi ukaomba kupita kiasi. "Basi, nataka wanaume wasali kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo tashwishi. . .?. . ." Na tuombe.

39 Yesu mpendwa, Mwandishi wa Neno la Uzima—Nawe ndiwe hilo Neno—tunakuja Kwako kwa kicho baada ya maelezo ya hilo ono ambalo, Mungu, unanishuhudia ya kwamba ni kweli. Bwana Yesu, naomba ya kwamba Wewe utayapa upako maneno haya usiku huu yakasikiwe na kila sikio linaloongozwa na sauti ya Kiungu. Na ikiwa kuna mmoja hapa anayesikiza nchini kote, iwapo hawako tayari na hawajajitayarisha wakati huu kukabiliana na mwito wa wakati huu, ule Ujumbe kutoka kwa Mungu, kutubu na kujitayarisha; kwa kuwa Ufalme wa Mungu unakaribia. Tunaomba ya kwamba itakuwa hivyo kwao usiku wa leo, ya kwamba watakambiliana na mwito wa wakati huu.

40 Ee Mungu, ningeomba msaada, nikijua wajibu wake na maana yake na jinsi—itanibidi kujibu kwenye siku ya hukumu kwa yale yote ninayosema hapa na penginepo. Nisaidie nipate kuwa mwaminifu sana, Bwana, kwa yale yote nifanyayo au

nisemayo katika Neno Lako, lipate kuzaa matunda. Kwa kuwa kama agizo Lako lilivyokuwa, "Neno hili lisiondoke kinywani mwako, bali litafakari usiku na mchana, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa katika torati. Maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana. Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako." Bwana Yesu, ifanye hivyo usiku wa leo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

41 Ijumaa na Jumamosi kutoka saa 4:00 hadi saa 6:00 kwenye maskani kule Barabara ya 8 ya Penn kutakuwa na mashauri, majibu ya mafundisho, maombi kwa ajili ya wagonjwa, na kadhalika. Njoo moja kwa moja kule chini iwapo una swali lo lote, cho chote utakacho. Kutakuweko na watu kule ku—kuyashughulikia. Bwana awabariki!

42 Basi, kwa ajili ya kuanza ibada ya usiku huu, siwezi kutenda lo lote ila kuifungua moja kwa moja kwa ujumbe wetu. Hilo ndilo kusudi letu kuwa hapa. Na sasa, ndiyo sababu nimekuja tena. Na Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, nataka kukabiliana na lile swali kuu la wakati huu, kuhusu *Ndoa na Talaka* [LILE NENO LILILONENWA, Kit. 3 Nam. 13—Mh.]

43 Basi, katika Wagalatia 4:27, nataka kusoma maneno haya, 4:27 hata 31 yote pamoja.

> *Kwa maana imeandikwa, Furahi, wewe uliye tasa, usiyezaa; Paza sauti, ulie, wewe usiye na utungu; Maana watoto wake yeye aliyeachwa pekee ni wengi kuliko huyo aliye na mume.*
>
> *Basi, ndugu Zangu, kama Isaka sisi tu watoto wa ahadi.*
>
> *Lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyomwudhi yule aliyezaliwa kwa Roho, ndivyo ilivyo na sasa.*
>
> *Lakini lasemaje andiko? Mfukuze mjakazi na mwanawe, kwa maana mwana wa mjakazi hatarithi kabisa pamoja na mwana wa mwungwana.*
>
> *Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana.*

44 Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Neno Lake. Sasa, naamini hapa ya kwamba nachukua somo kama hili geni, lisilo la kawaida. Bali wakati mwingine twamwona Mungu katika nyakati za kipekee, njia za kipekee, na vitu vigeni. Kwa sababu Mungu si wa kawaida, nao wamtumikiao kweli kwa mioyo yao yote, humtumikia kwa njia za kipekee kwa mambo au njia za ulimwenguni. Somo hili linaitwa *Mbegu Haitarithi Pamoja na Kapi*.

45 Paulo hapa ananena habari za mzao halisi wa wale wana wawili wa Ibrahimu. Paulo mwenyewe anafurahia kujiweka mwenyewe katika uzazi wa mwungwana.

46 Sasa, tunajua ya kwamba Ibrahimu alikuwa na wana wawili kwa wanawake wawili mbali mbali. Mungu alimpa ahadi kwa Sara—au kupitia kwa Sara, ya kwamba Mwana atazaliwa, na Kwa Mwana huyu ulimwengu ungebarikiwa. Mataifa yote yangebarikiwa kwa ajili ya huyu Mwana. Na imeaminiwa kwa kawaida, hasa miongoni mwa Wayahudi ya kwamba hii ilikuwa Isaka, bali sivyo. Huyu Mwana aliyeahidiwa wa Ibrahimu ni Yesu, na ndiye wa Mzao wa Kifalme aliyeahidiwa Ibrahimu.

47 Bali Ibrahimu akiwa na wana wawili, mmoja kwa—kwa Hagai, aliyekuwa mjakazi wa mkewe, mjakazi wa Kimisri mrembo, mwenye uso mzuri, ambaye Ibrahimu alikuwa amemtoa Misri kwa ajili ya—apate kuwa—mjakazi wa mkewe. Naye Sara, akifikiri ya kwamba Mungu hangaliweza kutimiza ahadi Zake zote, alimwambia Ibrahimu amchukue Hagai mjakazi wake na amwoe (ambapo kuoa wake wengi kulikuwa halali siku hizo) na kumzalia huyo mtoto, na hivyo ndivyo Mungu alikuwa amepanga, ya kwamba yeye angepata mtoto kwa Hagai tu . . . Bali tunaona ya kwamba hiyo haikuwa hivyo.

48 Naam, tunafahamu pia ya kwamba Mungu hukamilika katika utatu. Sasa, Mungu hukamilika katika utatu. Neema ni tano. Saba ni ukamilifu, kama ulimwengu. Mungu amekamilika katika Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Huo ndio ukamilifu wa Uungu. Yote ni Mungu mmoja katika dhihirisho tatu za sifa za afisi moja—ama afisi tatu katika Uungu mmoja.

49 Naam, kuna utatu pia katika ukamilifu wa hatua za neema kwa kanisa: Kuhesabiwa haki, Kutakaswa, Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huko ndiko kuzaliwa upya. Jinsi tu uzazi wa kawaida unavyoonyeshwa kwa mfano. Ambapo mwanamke anapomzaa mtoto, kitu cha kwanza kutoka ni maji, damu, na halafu uhai. Biblia ilisema katika 1 Yohana 5:7—ama 7:5, naamini ndivyo—ilivyosema, "Wako watatu washuhudiao Mbinguni, Baba, Neno (ambalo ni Mwana), na Roho Mtakatifu; hawa watatu ni Mmoja. Wako watatu washuhudiao duniani: Neno—maji, damu, na roho—maji, damu, na roho; na watatu hawa hupatana kwa habari moja."

50 Sasa, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni Mmoja. Hauwezi kuwa na Baba pasipo kuwa na Mwana; hauwezi kuwa na Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu. Bali unaweza kuhesabiwa haki pasipo kutakaswa. Unaweza kutakaswa pasipo kujazwa Roho Mtakatifu. Tulithibitisha hilo katika kanuni za maumbile.

51 Basi, wengi wenu huenda—huenda mimi ni mgeni kwenu. Nami—mimi sina elimu, nanyi bila shaka najua mnaelewa. Bali mimi hufundisha katika mifano, jinsi ya kawaida yanavyoonyesha ya Kiroho kwa mfano.

52 Basi, tunaona ya kwamba wako watatu katika ukamilifu. Mungu hukamilishwa katika utatu. Naam, na hivyo ilikuwa ukamilifu katika uzao wa Ibrahimu kulikuweko Ishmaeli, Isaka, Yesu: Ishmaeli akitoka kwa mjakazi, Isaka akitoka kwa mwugwana—na wote wawili kwa kujuana kimwili—bali Kristo Yesu akitoka kwa bikira, hamna kujuana kimwili.

53 Hapa huyu mzao, mmoja, Mzao mmoja, si wazao, bali Mzao mmoja. Hawa wengine hawakuwa mzao wa Ibrahimu, kwa maana Mzao wa Ibrahimu ulikuwa Mzao wake kwa imani ambao Mungu alikuwa akinena habari zake, si uzao wake wa kawaida. Kwa maana baada ya kifo cha Sara Ibrahimu alioa mwanamke mwingine naye akawa na wana saba pamoja na binti. Kwa hivyo haingalikuwa wazao wa Ibrahimu, ilikuwa Mzao wa Ibrahimu, mmoja. Na huyo alikuwa Mzao wa imani ya Ibrahimu, ikielekeza kwa Mzao wa kifalme ambaye angekuja kupitia kwa imani ya Ibrahimu, si maisha ya kawaida ya Ibrahimu, bali maisha ya kiroho ya Ibrahimu, aliyechukua kila lililokuwa kinyume cha Neno la Mungu na kuwa kana kwamba sivyo, naye akamwamini Mungu, akaamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa. Huyo ndiye Mzao halisi tunayenena habari zake.

54 Hapa tunaonyeshwa picha hata hivyo. Ule uzao ulianza, uzao wa ahadi ulianza kwa kushuku kidogo—kushuku ile ahadi ya asili. Je, waona jinsi inavyoanza hafifu kwa kutilia shaka ile ahadi ya asili? Mungu alimwahidi lbarahimu kupata mtoto huyu kwa Sara. Bali sasa tazama, ule uzao wa kwanza wa Ibrahimu kwa mjakazi ulikuja kwa ajili ya Sara kutilia shaka kwamba hili lingetendeka, kwa maana alikuwa mzee na amepita umri wa kuzaa.

55 Sasa, hivyo ndivyo kanisa linavyoanzia. Hivyo ndivyo linavyoanzia kila mara. Unaanza chini kabisa. Huanzii kule juu kabisa. Mtu anapojaribu kupanda ngazi akijaribu kufikia juu kabisa kwanza, atavunjika shingo. Huna budi kuanza mwanzo na kuendelea kupanda juu. Nasi hapa tunaona ule mwanzo wa ahadi ya Mungu ukidhihirishwa kwa mpango wa Mungu uliotiliwa shaka kidogo, na ukakatizwa.

56 Vivyo hivyo ndivyo dhambi ilivyoanza katika bustani ya Edeni. Hivyo ndivyo mauti yalivyoanza kwa dhambi, ilikuwa wakati neno moja la Mungu lilipoeleweka vibaya, au kutiliwa shaka. Huwezi kushuku au kuweka mahali pasipofaa neno moja la Mungu ambalo ni BWANA ASEMA HIVI...?...Neno liwe hivyo.

57 Na hapa hata Sara ambaye kwake ahadi...Sara akiwa mwanamke (ambaye ni mfano wa kanisa) alishiku mpango asili wa Neno la Mungu lililoahidiwa, na kusema, “Ewe, Ibrahimu, mume wangu, mchukue huyu mjakazi mrembo ukaishi naye, na ukawe mume kwake. Naye Mungu atatoa huyu mzao aliyeahidiwa kupitia kwake; nami nitamchukua huyo mtoto.”

Mwaona, kutojali nukta moja tu kulibadilisha mpango ule wote. Kwa hivyo hatuna budi kuchukua kila neno la Mungu kama BWANA ASEMA HIVI. Kila neno la Mungu ni kweli.

58 Ndiposa hapa uzao unaanza hapa katika ahadi iliyotiliwa shaka kidogo. Isaka akiwa mzao wa mwungwana, mwanamke aliyeahidiwa, akazaa—kama Paulo anavyojaribu kueleza hapa katika Wagalatia—akazaa mbegu ya kawaida, iliyoahidiwa. Naye anaendelea kusema hapa ya kwamba wa—watoto wa mjakazi hawawezi kurithi pamoja na watoto wa mwungwana, kwa sababu wao ni tabaka mbili mbali mbali. Na hiyo ni kweli. Asiyeamini hawezi kurithi pamoja na anayeamini. Haiwezekani kamwe.

59 Hapo ndipo shida ilipo leo. Hauwezi ukamfanya kuku wa kidhehebu akaamini pamoja na tai. Hauwezi kamwe. Hapo ndipo shida ijapo. Huna budi kuamini kila Neno la Mungu. Wewe, ninyi si warithi pamoja wala hau—hautaweza kujiunga nalo. Hauwezi. Huna budi kuwa tai au kuku.

60 Haingaliweza kurithi pamoja na Ishmaeli, uzao huo wa mjakazi wa—kwa ajili ya kutilia shaka. Sara alishuku Neno la Mungu, ya kwamba Mungu angaliweza kulitimiza. Tazama Ibrahimu (mnaona ninayojenga kwa ajili ya Jumapili asubuhi)—Ibrahimu hakuishuku. Sara aliishuku. Ilikuwa ndiye. Si Adamu aliyeishuku, ilikuwa ni Hawa aliyeishuku. Ndiposa, tutaona mengi juu ya hilo tutakapolichukua tena Jumapili asubuhi.

61 Wala ya Kiroho haiwezi—yenye tabia ya asili irithi na ya Kiroho. Wala wana wa Ishmaeli hawatarithi pamoja na—na wana—wana wa Isaka, wala wa kimwili kurithi pamoja na wa kiroho.

62 Kanisa la kimwili, kanisa la kiroho. Kuna kanisa la kimwili ambalo hawa wanawake wanaonyesha kwa mfano, na kuna Kanisa la Kiroho pia. Kwa hivyo kanisa la Kimwili na Kanisa la Kiroho hayawezi kurithi pamoja. Ni tofauti, ni ya nyakati mbili mbali mbali, watu wa tabaka mbili mbali mbali, chini ya agano mbili mbali mbali.

63 Hiyo ndiyo sababu kunyakuliwa ni tofauti na kutakuwa tu kwa ajili ya Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Hakuwezi kuwa kwa ajili ya uzao wa asili na wa kimwili wa kanisa. Hapana budi kutakuwa wa Uzao wa Kifalme wa Neno la Mungu kupitia kwa Ibrahimu, Uzao wa Kifalme. Hiyo ndiyo sababu kunyakuliwa kutatukia kwanza, kwa maana kumbuka, "sisi tulio hai, tutakaosalia, hatutawazuia, hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa maana parapanda ya Mungu italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuka, kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani." Tazama, na pia imeandikwa, "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu."

64 Kwa hivyo, hao si—hawatarithi pamoja; hawatanyakuliwa pamoja. Bila shaka kuna kanisa la kawaida na Kanisa la Kiroho, kanisa la kimwili, Kanisa la Kiroho.

65 Hapa. . .Unaona, hapa hamna. . .Hamna hukumu juu yao walio Uzao wa Kifalme, wa Kiroho, Uzao uliochaguliwa tangu awali wa Ibrahimu, kwa sababu wamechaguliwa Uzima wa Milele tangu awali. Wao wamekubali dhabihu ya Mungu iliyotolewa, na Dhahibu hiyo ambayo ni Kristo, Neno. "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu sasa (Yohana Mt. 5:24, mkitaka Andiko hilo). . .Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu (Warumi 8:1). . .Wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." Na Warumi 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu (Neno hilo hapa ni 'afahamuye.' Mlevi ye yote anaweza kulisikia, na kuondoka aende). . .Bali yeye alisikiaye Neno Langu—anayefahamu Neno Langu—na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ndio bwana! Yeye ambaye hii siri kuu ya Mungu imejulikana kwake, anafahamu, jinsi Mungu alikuwa katika Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, jinsi ambavyo Yeye na Baba ni Mmoja, jinsi zile siri kuu za kutimilizwa Kwake Mungu akijipeleka na kujileta Mwenyewe, akadhihirishwa katika nyakati za binadamu, na katika uzao wa wanadamu, na kuishi na binadamu, kudhihirisha Neno Lake siku hizo kwenye mapambazuko ya jua mashariki na kutenda jambo lilo hilo kama jua linavyotua magharibi, kujidhihirisha Mwenyewe katika Kanisa Bibi-Arusi, Neno lililodhihirishwa. Mwaona? Itakuwa ku. . ."Yeye afahamuye (hiyo ni, kuelewa), aliyefunuliwa Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele naye haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

66 Ule mzao wa kawaida ulikuwa tu mbebaji wa ule wa Kiroho—Mbegu, kama ubua, kishada, na kapi. Tumepitia hayo hapo mbeleni katika ujumbe mwingine, bali ningetaka tuyapitie kidogo tena—ama kuyarudia tena kwa dakika moja.

67 Basi, hapa mna hatua tatu za mbegu, zinatuonyesha picha halisi, hizo hatua tatu za mbegu ya kawaida ardhini. Kama vile mbegu hupandwa, inatoa ubua, jani dogo linachipuka kwake, kisha kishada, halafu mbelewele zinaning'inia mle, halafu kapi, ndiposa ile mbegu tena.

68 Tazama hatua hizi za mfano mkamilifu hapa na jinsi ulivyotimilika kabisa katika mfano, maana Mungu ndiye Mwanzilishi wa maumbile yote. Kwa hivyo maumbile hayawezi kushindwa kama tu vile Mungu hawezi kushindwa, kwa sababu ndiye aliyeweka kitu hicho katika hali yake tu—tupate kutazama na kuona.

69 Tazama, Hagai alikuwa ubua, ambao ulikuwa chanzo cha kuchipuka kwa ile mbegu. Sasa, haukufanana hata kidogo na ile mbegu. Ulikuwa ubua, kwa maana alikuwa mjakazi, hakuwa katika ile ahadi kamwe, hana uhusiano wo wote na Neno, mpagazi tu wa ile mbegu.

70 Mwangalie Sara, kile kishanda, kilichokuwa na mbelewele. Taifa hilo la Kiyahudi lilitoka kwake, kutoka . . .?. . . kutoka kwa Sara akaja Isaaka, kupitia Isaaka akaja Yakobo, Yakobo akawazaa wale wazee, na kupitia kwa wale wazee likainuka taifa.

71 Bikira Mariamu, imani, akazaa Mzao Neno wa Kiroho wa kweli aliliyefanyika mwili. Mwaona? Wanawake watatu, wanawake watatu walioibeba hiyo mbegu. Mmoja wao kusema kweli alikuwa uzinzi chini ya kuoa wanawake wengi. Wa pili alikuwa mwungwana, na wa tatu haikuwa kujuana kimwili kamwe, bali kwa imani aliamini Neno la Mungu. Hagai, Sara . . . Wote wawili Sara na Hagai ilikuwa kujuana kimwili, bali Mariamu alikuwa bikira kwa uweza wa Neno lililoahidiwa la Mungu. Hiyo ni kweli!

72 Ule ubua, Hagai . . . Wake wawili wakashuku ile ahadi, bali tazama kile hiyo ilisababisha. Wakati Hagai, mke wa pili wa Ibrahimu, ambaye alikuwa tu—bila shaka alikuwa mke suria . . . Bali akamzaa mtu. Lakini ni mtu wa aina gani? Biblia ilisema alikuwa mtu mkali sana. Aliishi kwa upinde wake na hamna mtu angalimshinda. Alikuwa mtu asiyetiishwa, mkali, asiyeweza kuongoka, asiyefanywa upya. Hangetiishwa. Alikuwa mkali sana, kwa sababu alikuwa kinyume cha Neno la Mungu. Cho chote kilicho kinyume, mhubiri ye yote, mshirika ye yote, kanisa lo lote, ambalo ni kinyume cha Neno la Mungu litazaa kundi jeuri na zinifu la Hollywood ya kidunia lisiloweza kudumu kwa Neno lisilochanganywa, kwa sababu hata halijahesabiwa katika ile ahadi. Hata!

73 Sara, yule mke wa kweli wa ahadi, akiwa kishada, akazaa mtu mpole. Mahali pake akazaa taifa lililoahidiwa ambalo lilimtumikia Mungu. Bali Mariamu bila kujuana kimwili kamwe, bali aliamini Neno lililoahidiwa alipokuwa bikira, asiyemjua mwanamume. Naye Malaika wa Bwana akakutana naye, kasema, “Salamu, Mariamu, umebarikiwa wewe katika wanawake, kwa maana Mungu yu pamoja nawe.”

74 Naye akasema, “Yatakuwaje mambo haya?”

75 Yeye—yeye akasema . . . Malaika akasema, “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako.”

76 Haikuwa imetendeka katika nyakati zote, bali Mariamu alimwamini Mungu. Naye akasema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana.” Yeye akaamini Neno. Atampataje? Alijua ya kwamba Hagai alimpata mwana kwa tamaa ya kujuana kimwili na Ibrahimu naye Sara alimpata mwana kwa tamaa

ya kujuana kimwili na Ibrahimu—watoto wa ahadi, mjakazi na mwungwana—na hapa anaulizwa kuamini lile toleo kwa imani aliyokuwa nayo Ibrahimu ambaye aliamini mambo yasiyowezekana; "Mradi tu Mungu alisema ilikuwa hivyo, hiyo inaifanya kweli!"

77 Yeye akamwamini Mungu, hakuionea mashaka. Alisema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana. Haijalishi nitalaumiwa vipi na ulimwengu, na iwe kwangu kama ulivyosema." Hapo akazaliwa yule Mzao halisi.

78 Sara hangalifanya hivyo, kwa sababu ilikuwa kujuana kimwili. Naam. Wala Sara hangaliweza, kwa maana ilikuwa kujuana kimwili, wala kanisa haliwezi chini ya ufuasi wa kidhehebu; inachukua imani safi kabisa ya Neno la Mungu kufanya ahadi izae watoto. Ufuasi wa kidhehebu hautazaa kamwe kanisa lililozaliwa mara ya pili. Hauwezi. Utazaa kitu kingine cha kuigizwa. Utazaa kitu—utazaa kitu fulani ambacho kinaliigiza, kitu kinachojaribu kuwa kama lenyewe. Bali Kanisa halisi la Mungu lililozaliwa mara ya pili huamini Neno Lake dhidi ya cho chote kile, kwa sababu halijaghoshiwa. Mambo haya huja kwa ahadi ya Mungu.

79 Mariamu, aliyekuwa wa kweli, alisema kwa—bila kujuana kimwili—kasema, "Na iwe kwangu kama ulivyosema. Tazama, mimi ni mjakazi Wako." Naye akazaa... Alizaa nini? Si mtu mkali sana, si taifa, bali alizaa Neno, Mungu Mwenyewe aliyedhihirishwa katika mwili (Amina!), yule Mzao wa kweli wa Mungu aliyedhihirisha kila ahadi ambayo Mungu alifanya katika Biblia. Bila Yeye hamna mtu awezaye kuishi—bila Yeye. Alikuwa ile mbegu ya kweli. Alikuwa tayari amepita lile... Alikuwa kapi lililozaa ile punje.

80 Sasa, wale wengine wawili walikuwa wabebaji wa uhai, kama tu uzao wa kawaida. Mariamu... Sasa kumbuka, nilisema wale wengine wawili... Sasa, Mariamu, usimfanye yeye Mungu, jinsi watu wengine hujaribu kumfanya. Yeye hakuwa Mungu. La, bwana! Alikuwa tu mchukuzi wa ile mbegu kama wengine wao walivyokuwa.

81 Bali kama vile imani katika Neno inaleta zaidi sura halisi, kama vile mahindi yanavyoiva, ama ngano. Ubua huchipuka; ndipo mbelewele; kisha hutokea kapi. Bali wakati... Unafikiri... Hilo kapi, usipokuwa mwangalifu, litaonekana kama ngano halisi hasa. Bali linapofunguliwa, ngano halisi imo ndani yake. Ni chukuzi tu tena.

82 Kwa hivyo unaona Mariamu, si kwa kujuana kimwili, bali kwa imani, kitu kama hicho hasa... Mariamu hakuwa yule Mzao. Mariamu alikuwa mchukuzi wa yule Mzao. Yeye alikuwa ndiye Mzao wa imani wa kweli, kwa sababu Neno la Mungu lilitolewa kwa Ibrahimu ni kwa imani. Na ni imani tu ambayo

inaweza kuleta yale Mungu alisema angetimiza, imani katika Neno Lake.

83 Tazama, jinsi Mariamu alikuwa kama ile halisi, bali kama kapi. Kapi huikumbatia hii mbegu kwake yenyewe, na kuikinga, na kuilea, hata itakapojitegemea, ikaive. Vivyo hivyo wakati huu wa tatu wa kanisa la Kipentekoste uliiva huku umeshikilia mbegu hii hata utakapofika wakati wa kufunguliwa kwa lile kapi. Mariamu akiwa mama wa Kristo, mtambo tu wa kuatamia mayai. Yeye hakuwa damu ya Mariamu; hakuwa damu ya Kiyahudi; hakuwa damu ya Mataifa; Yeye alikuwa Damu ya Mungu. Mungu aliumba hii Damu. Haingekuwa kujuana kimwili. Yeye hakuwa Myahudi wala Mtaifa.

84 Mtoto mchanga hana hata tone moja la damu ya mamaye. Damu hutoka kwa baba. Tunajua zile chembechembe za damu kuwa katika mwanamume. Kama vile kuku, hawezi kutaga mayai, kuku anaweza, bali iwapo hakuwa pamoja na kuku wa kiume, jimbi, hayataanguliwa. Halianguliki, ijapokuwa linafanana kabisa na yai la kuanguliwa. Maumbile yake yote yamefanana nalo, bali halina uhai dani yake.

85 Hivyo ndivyo ilivyo kwa watu wanaomkiri Kristo. Wengi wao huonekana kama Wakristo, hujaribu kutenda kama Wakristo, bali huna budi kuwa na Kristo ndani yako, ambaye ni Neno lililodhihirishwa, kama sivyo haitakomaa kamwe kama Mkristo halisi anayeamini Biblia. Itakuwa daima kitu fulani cha kidhehebu. Haiwezi kuishi, maana hamna uhai kwake kuishi. Yai haliwezi kuanguliwa, linaozea kiotani iwapo halijakuwa pamoja na—na ndege wa kiume.

86 Kama tu wafuasi wa Kanisa. Unaweza ukawalea na ukawaita—ukawafanya mashemasi na cho chote kile, bali hawa—utakuwa na kiota kilichojaa mayai yaliyooza isipokuwa yameungana na mbegu ya kiume. Naam!

87 Mchukuaji, lile kapi, liliilea. Hiyo ni kweli. Ndipo hiyo, hivyo ni kusema, Mbegu Yenyewe haina budi kuliacha lile kapi, au kapi sharti liachilie ile mbegu kusudi hiyo mbegu ipate kuwa kwenye jua ili ikaivishwe. Tunaona yote katika mifano.

88 Tazama hapa jinsi ilivyo karibu, kanisa la siku za mwisho linafanana na Mbegu Yenyewe. Tazama jinsi hili dhehebu la Pentekoste lililoinuka katika siku za mwisho—na tutaifafanua baada ya kitambo kidogo, mwaona—jinsi wanavyokaribia sana kufanana na ile Mbegu. Kapi linapotokea kwenye punje ya ngano—ama jani la ngano, baada ya mbelewele kuingia mle katika sehemu ya pili na kuleta sehemu ya tatu, ambayo ni—ni ni kapi. . . Na jinsi, iwapo wewe huchunguzi kwa makini sana hautaweza kamwe kujua kwamba hiyo si punje halisi ya ngano mle ndani. Hiyo punje dogo inapochipuka, huonekana kama punje. Bali hebu uketi chini ukaifungue, na utaona kwamba hamna punje kamwe. Ni kapi tu, mchukuzi wa punje.

Naam, punje hutoka kwa hilo. Lakini hamna nyingine tena baada ya hilo kapi. Kumbuka, hamna Mzao zaidi ulioahidiwa kwa mwanamke ye yote po pote baada ya Mariamu. Na hamna madhehebu yaliyoahidiwa baada ya Pentekoste. Ni Bibi-Arusi anayenyakuliwa anayetoka humo, ile mbegu, Neno lililodhihirishwa tena.

89 Tazama, uona zinavyofanana. Mathayo ilisema—Mathayo Mt. 24:24, ilisema kwamba hizo roho mbili katika siku za mwisho, roho ya kanisa ya watu wa kanisa na Roho ya watu wa Bibi-Arusi, zitafanana sana hata ingewapoteza, kama yamkini, walio Wateule. Hivyo ndivyo jinsi zinavyofanana.

90 Tazama jinsi ilivyokuja kupitia kwenye ubua. Sasa, tazama, tutanyosha jambo hapa kwa mfano. Luther katika ule wakati wa kanisa akizaa yule Mzao Bibi-Arusi ilikuwa roho yule yule. Luther alisimama tu juu ya punje moja ya mbegu; hiyo ilikuwa kule kuhesabiwa haki kwa imani. Alikuwa mfano halisi wa Hagai, yule ubua. Tazama, Wesley alikuwa mfano wa Sara, Filadelfia, ule wakati wa upendo, uliochipuza kishada ambacho . . . Katika Wakati wa Wesley kulikuweko wamishenari wengi kuliko wakati mwingine wo wote tumekuwa nao. Ule wakati mashuhuri sana wa umishenari wa siku za John Wesley . . .

91 Bali Pentekoste ilimwakilisha Mariamu, Mariamu, ile sehemu yake ya mwisho. Sasa, yeye hakuwa yule Mzao, walakini ule uhai wa yule Mzao ulikuwa ndani yake. Bali haukuwa umekomaa bado. Najisikia wa kidini sana. Haukuwa umekomaa bado. Ulikuwako, bali haukuwa umekomaa. Ndivyo ilivyo kwa wakati wetu wa Pentekoste tunamoishi. Hapana budi ku—kutokee Neno ambalo si la kidhehebu, nje ya milki ya hilo dhehebu.

92 Luther alifanyika kapi pamoja na neno lake la kwanza, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Wesley alikuwa na maneno mawili, utakaso; kazi ya pili dhahiri ya neema. Pentekoste ilikuwa na neno la tatu, kurudishwa kwa karama. Bali ile mbegu yote haina budi kutokea. Mnaona jinsi wao walivyounda dhehebu kwa neno moja, na neno lingine, na neno lingine. Bali hapana budi kuwa na kitu kisichoweza kufanyika dhehebu. Ni ule uhai wote uliomo mle ambao hauna budi kujizaa wenyewe katika Bibi-Arusi. Hapawezi kuwepo nyakati zingine za kanisa baada ya huu. Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu na dada. Tuko hapa; tumefika. Bwana ashukuriwe! Amina!

93 Naam, tunaona mambo haya ni ya kweli iwezavyo kuwa. Ndiposa tunaona, anapokuwa kishada, au Wesley akiwa kishada, kisha Pentekoste ikiwa kapi, ambayo ndiyo hatua inayofuata kwa kutokea kwa punje . . .

94 Bali ndugu, dada, ubua siyo punje; wala kishada sio mbegu, wala kapi si mbegu, ijapokuwa kila mara inapoiva

inafanana zaidi na zaidi na punje. Ubua haufanani na punje. Basi nini kinachochipuka? Kishada, kifundo kidogo. Kinaonekana—kinafanana sana na punje kuliko—kuliko jani linavyofanana nayo. Nini kinachofuata? Kapi. Kinashikilia ile punje; kinalea punje.

95 Sasa tazama tena kwenye ile ahadi Mungu aliyomfanyia Ibrahimu ya, "Uzao wako..." akinena kiroho. Ye yote wetu anajua hayo. Alikuwa akinena kuhusu Kristo, si Isaka. Kupitia Mzao wake wa imani.

96 Tazama, wa kwanza alikuwa kwa mjakazi. Hakufanana hata kidogo na ile ahadi. Mungu si lazima aghairi Neno Lake kwa ajili ya mtu ye yote. Mungu alisema itakavyokuja, na hivyo ndivyo itakavyokuja. Bali Sara akiwa mwakilishi wa kanisa, mfano wa Kanisa, ali—alitambua hapo kwamba, ya kwamba... Yeye alisema, "Vema, naamini ni tukio la ajabu sana. Hata siwezi kuliamini, kwa hivyo wewe nenda kamchukue Hagai, ukamfanye mkeo." Unaona hapo? Huo ubua haufanani na ile ahadi kamwe, bali Sara alipojitokeza. Naam, hiyo ilionekana zuri sana. llifanana sana na ile ahadi hapo, bali haikuwa ile ahadi halisi, kwa sababu Israeli katika Isaka ilishindwa na ikamkana yule Mzao halisi alipokuja (Haleluya! Msihangaike; msitimue mbio. Hilo halitawadhuru!)—ikamkana yule Mzao, ikamsulubisha, na kumtundika msalabani.

97 Jinsi Paulo alivyosema hapa, "Je! si—si mzao wa—wa mwungwana ama mjakazi alimuudhi Mzao wa mwungwana?" Vivyo hivyo uzao wa dhehebu huiudhi ile punje halisi. Haina budi kuwa hivyo daima. Hawatarithi pamoja. Hawatachangamana. Hao bila shaka ni ahadi mbili mbalimbali, nyakati mbili mbalimbali, tabaka mbili za watu mbali mbali kabisa. Mmoja ni Bibi-Arusi na mwingine ni kanisa. Wanahitilafiana kabisa.

98 Walakini wao si ule uzao ulioahidiwa kuja. Wala hata Sara; wala—wala Hagai. Wala Sara hakuwa huyo—au wala Mariamu hakua huyo Mzao. Mariamu hakuwa yule Mzao. Yeye alikuwa mchukuzi wa huyo Mzao. Bali aliulea, akauzaa kwa tumbo lake la uzazi, jinsi tu nalo kapi lilivyozaa kwa tumbo lake la uzazi ile Mbegu halisi. Bali kapi siyo Mbegu. Hiyo ni...lkaribu zaidi na mbegu. Imeikumbatia Mbegu. Kule nyuma kwenye ubua, uhai unatawanywa kote ubuani. Na inapofikia kwenye mbelewele, unakusanywa karibu pamoja. Lakini inapofikia kapi, uko mle ndani kama mbegu, na unaumbika kama mbegu kabisa. Yesu alitwambia itakavyokuwa katika siku za mwisho: zitafanana sana hata ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini. Ndiposa mbegu huondoka humo. Nayo kapi, uhai unaondoka kwenye kapi. Nayo kapi ni chukuzi. Na hivyo ndivyo madhehebu yetu yamekuwa, ni wapagazi. Luther, Wesley, Pentekoste, na sasa ndio wakati wa kutokea kwa mbegu.

99 Tazama, tazama tu. . .Yeye hakuwa yule Mzao; Mariamu hakuwa hivyo—kapi tu, kishada, na ubua, wapagazi wa sehemu ya Neno, si Neno lote. Luther ana kuhesabiwa haki. Wesley alikuwa na kutakaswa, Pentekoste wana kule kurudishwa kwa zile karama. Bali Neno lilipokuja. . .Sasa, wanaweza kuleta hilo, ya kwamba kuhesabiwa haki kutamwokoa mtu. Unaamini hilo? Naam! Ni chukuzi la Neno, jinsi ninavyoamini ya kwamba ubua ni sehemu ya ngano. Naam! Bali ni chukuzi. Siyo ule uhai. Ndipo kutakaswa kunakuja. Wangapi wanaamini katika utakaso? Iwapo unaamini Biblia huna budi kuuamini. Naam! Kwa hivyo hiyo ingali si. . .Inafanana zaidi kidogo nayo. . . Hayo ni maneno mengine mawili. Ndiposa ikaja Pentekoste, kule kurudishwa kwa zile karama. Kunena kwa lugha, wakakuita thibitisho mathubuti la Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha. Hapa wakaiita hiyo thibitisho mathubuti, iliyozaa nini? Kapi. Bali wakaunda dhehebu. Bali unapofikia kusema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja," na mambo haya mengine, ndipo kapi linajiondoa kwake. Bali Kanisa Bibi-Arusi halisi atazaa Neno nzima la Mungu katika utimilifu Wake miongoni. . .?. . .kwa maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

100 Tazama, ndani ya tumbo la uzazi la Mariamu mlikuwemo yule Mzao. Bali yule Mzao alipozaliwa, Yeye alisema, "Mimi nimekuja kufanya mapenzi Yake aliyenipeleka. Mimi na Baba Yangu tu Mmoja. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini." Mzao yule ndiye huyo. "Ni nani miongoni mwenu anihukumiaye kutokuamini? Yale Biblia iliahidi ningetenda, tayari nimetenda. Mungu amethibitisha hayo kupitia kwangu!" Akasema. "Ni nani angeniambia sasa, mzao. . . " Bali yule Mzao katika Mariamu, lile kapi, lilikuwa karibu kuwa hiyo, bali sivyo. Alikuwa angali katika tumbo la uzazi.

101 Tazama. Na katika wakati wa Pentekoste, kupitia kwa wakati wa Wesley, imekuwa jambo lile lile hata wakati huu wa Pentekoste. . .Sasa tazama, bali katika kule kufunguliwa kwa ule Mhuri wa Saba, Ufunuo 10, lile Neno lote litazaliwa katika kudhihirishwa tena na kuthibitishwa na Roho wa Mungu katika nguvu zote, kama ilivyokuwa Yeye alipokuwa hapa duniani, akidhihirishwa vile vile, akitenda mambo yale yale aliyotenda alipokuwa hapa duniani. Amina! Waebrania 13:8 ilisema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Katika Luka 17:30 Yesu alisema, "Katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma Mwana wa Adamu atakapokuwa akijifunua Mwenyewe tena, itakuwa jambo lile lile."

102 Ulimwengu umo katika hali ya Sodoma na kanisa limekwenda Sodoma pamoja nao kama Lutu na mkewe. Na kama nisemavyo kuna Kanisa lililoteuliwa mahali fulani ulimwenguni lililotoka na kujiweka mbali na mambo hayo. Na madhihirisho ya Mungu yamelivutia macho. Tumo katika siku za mwisho.

103 Kapi limetoa uweza wake kwa ile mbegu; likaondoka. Lilikuwa kapi zuri, bali limemaliza kazi yake.

104 Mnaona, ni Bibi-Arusi Neno wa Bwana Arusi Neno. Ile mbegu asili ya Ibrahimu, Isaka, na Yakobo na—au mbegu asili, hasa, ya Ishmaeli, mbegu asili ya Isaka, na kadhalika, ilipaswa kuingia ardhini kusudi i—ikazae hii nyingine, ikamlete Yesu. Na vivyo hivyo hawa wengine wote. Hizi mbegu hazina budi kukauka—namaanisha, hizo kapi hazina budi kukauka na mbelewele hazina budi kukauka na kila kitu kife kusudi ile mbegu ipate kujizaa yenyewe.

105 Hivyo ndivyo imekuwa kila wakati, Madhehebu yamekuwa wapagazi wa sehemu yake. Sehemu yake ni Neno, kwa sababu imefichwa wale warekebishaji wenye hekima ama ku—imetiwa muhuri kwao hata wakati wa tai utakapowadia. Biblia ilisema hivyo. Naam, bwana! Bila shaka tumeahidiwa hayo katika Malaki 4. Naam, ndivyo. Yeye ameyaficha wenye hekima na akili!

106 Na ndiyo kwanza tumekwisha kumaliza Kitabu cha Ufunuo, tunaona ya kwamba kila—wajumbe hao wote watatu, au wale wanyama waliojitokeza, kila mmoja wao alikuwa sawasawa na Luther kabisa. Kila mmoja alichukuana na mwingine kabisa, ambao ni ndama na wanyama mbalimbali wa Biblia. Ikaingia kwa kuhesabiwa haki, kutakaswa, hata kufikia Wapentekoste; bali wa nne alikuwa tai. Hiyo ni kweli, na kupitia kwa wakati huo Mungu akamwinua. Kwa hivyo haina budi kupitia wakati huo kusudi iwe kweli. Naam, bwana, ahadi ya tai inatimizwa ya—ya Malaki 4.

107 Yesu hakuwa wa Mariamu, bali alipitia kwa Mariamu, kama ule uhai unavyopitia kwa kapi.

108 Sasa, wengi wenu ndugu na dada wazuri Wakatoliki usiku wa leo huenda mkafikiri ya kwamba Mariamu alikuwa mama ya Mungu, jinsi msemavyo. Angekuwaje mama wa Mungu, naye Mungu hana mwanzo wala mwisho? Mwaona? Basi ni nani aliyekuwa Baba Yake Mungu iwapo yeye alikuwa ndiye mamaye? Mwaona? Mungu alikuwa Muumba wa Mariamu, naye Mariamu hakuwa muumba Mungu. Yeye alijiumba Mwenyewe katika tumbo la uzazi la Mariamu, si uumbaji wa mwanamke mwenyewe. Ilikuwa...Mungu alijiumba Mwenyewe. Yeye hakuwa wa Mariamu, bali Mariamu alikuwa Wake. Naam! Biblia inatufundisha ya kwamba vitu vyote viliumbwa Naye. Na hamna kitu kilichoumbwa ila kile kilichoumbwa Naye. Kwa hivyo ingaliwezekanaje...?...Angalikuwaje na mama huku Yeye akiwa Mungu Mwenyewe?

109 Sasa, twaona hapa ufunuo wa kweli wa mfano wa kweli. Kuna wachukuzi watatu wanawake hata ilipokomaa ikawa Yesu. Jinsi Ishmaeli hangaliweza, kwa sababu bila shaka alizaliwaa—jinsi tungefikiria siku hizi—nje ya ndoa, kwa maana alikuwa

mwana wa mjakazi. Ndipo ikafanana kidogo zaidi Naye, kama Yesu, ambaye ilitoka kwa Isaka. Bali siyo bado, kwa sababu ilizaliwa kwa kujuana kimwili kati ya Sara na Ibrahimu. Ndipo basi akaja Mariamu, kwa uzazi wa kibikira akamzaa Yesu Kristo (naam!), Mungu, Neno lililofanyika mwili.

110 Sasa tazama, kulikuweko wanawake watatu. Ndio hao wanawake watatu walioonyeshwa hapa kwa mfano, makanisa (wanawake daima huwakilisha makanisa) maana yake ni nyakati tatu za kidhehebu, wachukuzi, ambazo pia hazina budi kufa na kukauka, kama tu vile kapi na kadhalika hufanya, kutoa nafasi kwa ile mbegu. Mbegu haiwezi iva—haiwezi kuiva, hasa, hata kapi, ubua, majani, vyote vimekauka. Hivyo ni kweli. Hufyonza kila chembe ya uhai kutoka kwao. Amina! Yote ilichokuwa ni hayo na kuongeza. Havingeweza kulifanya.

111 Sasa, ni wakati wa mbegu au wakati wa Bibi-Arusi. Makapi yamekufa, yale makapi tayari yamekwisha kukauka. Ni wakati wa Neno bikira, lisilogoshiwa . . . Ni bikira. Kumbuka, wakati wa Neno bikira. Ukiliweka mikononi mwa madhehebu, bila shaka halitakuwa bikira. Litakuwa limeguswa-guswa na watu utakapolifikia. Bali Kanisa la Mungu halijaguswa na dhehebu (haleluya!); Ni Neno la Mungu lililozaliwa kibikira, lililodhihirishwa, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo na hata milele. Haleluya! Ni—ni ajabu jinsi gani! Nalipenda. Naiamini. Najua ya kwamba ni Kweli. Halitaguswa. Hapatakuweko kuguswa-guswa na watu wa kidhehebu katika kuzaliwa kibikira kwa Bibi-Arusi. Hasha, bwana! A—ameamriwa na Mungu kutoka kwa kitu kama hicho. "Msiguse vitu vyao vichafu . . . wamekuwa miewe."

112 Inanikumbusha. Nilikuwa nikija kutoka Phoenix hivi majuzi, kuja Tucson kwa ajili ya mikutano, Roho wa Mungu akanitazamisha kitu fulani (mimi na mke wangu tulipokuwa tukizungumza. Nao watoto wamelala upande wa nyuma wa motokaa, usiku unaingia), akanitazamisha kengewa. Nami nikamwangalia huyo kengewa kidogo na kumchunguza. Yeye ni mfano mkamilifu kabisa wa kanisa siku hizi.

113 Sasa, kengewa, kama tujuavyo sote, amepoteza hali yake halisi ya uumbaji asili. Hiyo ni kweli kabisa. Zamani za kale alifanana na tai, nduguye mkubwa, kengewa alikuwa hivyo. Bali sasa haruki mbinguni kuwinda mana yake ya kimbinguni, bali amekuwa mdhaifu. Haruki tena mbinguni; hurukaruka ardhini kama mwewe, huketi juu ya miti ya simu, hurukaruka akitafuta sungura waliokufa. Kengewa hakuumbwa kufanya hivyo. La, aliumbwa akafanane na tai. Sasa, hiyo ni kama tu kanisa. Lilifanywa likafanane na tai. Linapaswa kuchukua mahali pake mbinguni. Bali badala ya kufanya hivyo, limekuwa dhaifu. Halipuruki hata kusikojulikana tena, mawinguni. La, bwana! Linategemea njia zake za kisasa za mwingizo, za elimu, na theologia ya dhehebu lililoundwa na mwanadamu, wakitafuta

mizoga ya sungura waliooza ambao walikuwa wameshikwa na kitu kingine (naam!) . . . kurukaruka ardhini. Hiyo ni kweli! Kengewa. Mnaona hivyo ndiyo inayoonyosha. Tai hajabadilika hata kidogo. Yeye hudumu tai.

114 Yeye haruki angani, kengewa hafanyi hivyo tena, kuwinda mana yake kule juu, bali hutegemea mizoga anayopata. Kengewa hawezi . . . ? . . . mti wa ua kuruka chini . . . Bali mtazame maskini kengewa leo. Tembea barabarani, utaona waya za simu zimejaa kengewa, wakitumaini kupata kitu—kitu kilichouawa, kitu kilichooza. Amekuwa kama hana mabawa ya kutosha kuruka juu. Yeye ni . . . Muda si muda atakuwa ardhini, hawezi kuruka kwa sababu amekuwa mdhaifu. Hatumii tena nguvu zake alizopewa na Mungu.

115 Thibitisho lake maalumu lilikuwa aruke angani na kutazama chini. Bali sasa, yeye hushuka chini na hawezi hata kutazama juu. Hamu yake imo kwenye sungura wafu, kutafuta anachoweza kupata barabarani, cheche, komba, ama cho chote kile mtu fulani amekanyaga kwa motokaa. Yeye si tai, bali ni kitu kama tu. Jinsi tu kanisa linavyotegemea elimu na kadhalika kwa ajili ya chakula chake, mlo mfu uliokufa miaka mingi iliyopita kupitia kwa Luther, na Wesley, na Wapentekoste, na umeendelea . . . ? . . . Ni kutazama nyuma kwa kanuni za imani zilizobuniwa na mwanadamu, badala ya kuruka juu katika mbingu za Neno ambamo yote yanawezekana kwao waaminio.

116 Yeye amechukua tabia za nderi. Vitu vilivyokufa vilivyoachiwa mwewe, ulimwengu. Elimu na mambo kama hayo yaliachiwa ulimwengu, si Kanisa. Yeye amekuwa dhaifu sana hata . . . Yeye si chapuchapu tena. Hawezi kuruka hata mbingu zisizo laini ambamo lolote linawezekana kwa hao waaminio. Aliketi kitako na kusema, "Vema, Daktari *fulani wa fulani* alisema *fulani* . . . Dhehebu langu haliamini hivyo." Jamani, ewe kengewa aliyepotoka, anayeogopa kujitwalia ahadi za Mungu.

117 Unasema, "Vema, siku za miujiza zimekwisha." Wewe ni mdhaifu. Unaogopa kuchukua mbawa zako na kuruka kule ng'ambo, na je! umekuwa mdhaifu sana hata kwa mkutano wa maombi? Umefikia ambapo hata unaogopa kumaliza zaidi ya dakika kumi madhabahuni? Unarukaruka kama mwewe ukila mizogo ardhini. Naam, bwana!

118 Yeye ni mdhaifu sana kuruka kwenye zile ng'ambo zisizo laini tena. Anarukaruka kama mwewe, na anakula chakula cha mwewe (hivyo ndivyo ilivyo! Naam!), hata ameanza kufanana na mwewe. Hutenda kama mwewe, na si kengewa tena. Anafanana zaidi na mwewe kuliko kengewa. Kengewa anapaswa kuruka juu, si kuketi kwenye miti ya simu na kungojea sungura aliyekufa, na ndipo ashuke chini pale na kurukaruka juu chini barabarani kama mwewe. Mnaona?

119 Hivyo ndivyo tu kanisa lilivyo leo. “Ya nini kuruka kule juu kupurukapuruka kule huku naweza kupata sungura humu?” Lakini wamekufa wameoza; wameambukizwa. Wakati mmoja walikuwa wazuri. Vivyo, hivyo fundisho la Walutheri, Wesley, na Wapentekoste. Mbona unakula kama mwewe? Mana mpya ilianguka kila usiku kutoka mbinguni kwa ajili ya wana wa Israeli walipokuwa safarini. Yo yote iliyobakia iliambukizwa. Tulizoea kusema nchini, “imeingiliwa na mabuu.” Kuna mabuu wengi sana katika ujuzi wetu siku hizi. Dini zetu zinategemea yale mtu fulani alivyosema, aliyosema mtu fulani, na, “Hiyo ahadi ni kwa ajili ya wakati mwingine.”

120 Mtu fulani alinijia si muda mrefu uliopita, mhubiri Mbatisti, hapa nyumbani mwangu, na kusema, “Unajua,” kasema, “ningetaka tu kukusahihisha jambo fulani.”

Nikasema, “Lipi?”

Kasema, “Unajaribu kufundisha fundisho la kimitume humu katika zamani hizi,” kasema; “zile nyakati za kimitume zilikoma.”

121 Nikasema, “Lini? Nitakwambia zilipoanzia, nawe uniambie zilipokomea.” Nikasema, “Je, unaamini Neno?”

Akasema, “Naam.”

122 Nikasema, “Vema, Basi, kwenye ile siku ya Pentekoste, unaamini hapo ndipo zile nyakati za kimitume zilipoanzia?”

Akasema, “Naam.”

123 Nikasema, “Basi yule mnenaji, mtume Petro, alisema maneno haya. . . “Na kumbuka, Yesu alisema, ‘mtu ye yote akiondoa neno lo lote kutoka kwa Hiki au kuongeza Kwake, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima.’ Huyo ni mhubiri au mtu ye yote aliyeandikwa kwenye kile Kitabu.” Nikasema, “Petro alisema, ‘Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.’ Zilikoma lini basi? Zimekuweko daima.” Ni kundi la kengewa lililobadilika kuwa nderi na linarukarukia mizoga mingine iliyokufa waliyouliwa na kizazi kingine (naam!) si mana mpya itokayo mbinguni tena.

124 Hawalitaki. Hawawezi—hawawezi kuwa na ibada ya maombi. Kwanza hata si tai, watu hafifu, sio chapuchapu, hurukaruka huku na kule. Vivyo hivyo madhehebu yetu mamboleo hutegemea elimu ya theologia iliyobuniwa na wanadamu kueleza mambo haya yote. Nao hukubali hayo. Hawangechukua Neno lililosema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Hawatachukua Malaki 4. Na hawatachukua ahadi hizi zingine zote zinazohusu siku hii, na kusema jinsi

wakati huu wa kanisa—jinsi nabii alivyosema, "Itakuwa nuru wakati wa jioni." Hawachukui haya; wanataka kurukarukia yale dhehebu la Kipentekoste liliuwa miaka mia moja iliyopita, wakila mana iliyooza nusu. Naam! Haifai kitu!

125 Tazama, kanisa ni la kimwili sana, linajilisha nyama zilizooza za kidunia, vitu vya ulimwengu vilivyokufa, jinsi tu mwewe afanyavyo. Siasa za kanisa, hawamwachi Roho Mtakatifu alitumie kanisa mtu; inawabidi kwanza wafanye siasa waone kama dhehebu hilo litampokea ama sivyo. Hiyo ni kweli. Wao wanapenda ulimwengu. Wanavalia kama walimwengu. Wanafanana na walimwengu. Wanatenda kama walimwengu. Wao ni mwewe kama walimwengu. Ni wavivu, hafifu, wanaopatana. Hayo ndiyo yote walivyo. Je, umepata kuona tai akipatana? La, bwana! Yeye hapatani kamwe. Wala Mkristo halisi pia. Yeye si mtu mdhaifu. Yeye atawinda hata atakapoipata. Amina! Naam, bwana! Yeye atapata nyama yake. Yeye anataka mana mpya. Atafika kule na kuchimbua mpaka aipate. Ataruka juu zaidi na zaidi. Iwapo haimo kwenye bonde hili, ataruka juu zaidi. Kadiri urukavyo juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Kwa hivyo ni wakati wa tai wa siku hizi kuruka juu zaidi, wakachimbue kwenye ahadi za Mungu, si kuishi kwa chakula cha mwewe kilichouawa miaka mingi iliyopita. Tokeni kwake.

126 Siasa, kushinda kwa kura na kushindwa, wakisema *hivi, vile,* ama *vinginevyo*. Na Roho Mtakatifu si huru kamwe kuingia kanisani tena. Hamna tena ibada za maombi, hamna tena kumsihi Mungu sana apate kutimiliza Neno Lake. Hamna tena kuungama ya kwamba Neno ni lile lile jana, leo, na hata milele. Wameshuka chini kimwewe, wakaunda dhehebu, kaandika majina yao kwenye kitabu, wakawa wavivu na wadhaifu, na wakaketi pale wakisimbuliana juu baadhi ya mizoga fulani iliyooza. Ndiposa wanadhaniwa kuwa angalau kengewa ambaye ni ndugu anayefanana na yule tai, nabii aliyelileta Neno la Kweli na kulidhihirisha.

127 Wao hutegemea theologia iliyooza nusu, iliyobuniwa na binadamu. Anaipata kutoka wapi? Katika kijikaratasi cha taratibu za Shule ya Jumapili iliyobuniwa na mwanadamu aliyouliwa na mwanachuoni fulani kule kwenye seminari, inayomwambia, "Siku za miujiza zimekwisha; hamna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, haya yote ni upuzi." Wataka kuniambia kwamba tai angalikula hayo? Hawezi. La, bwana! Wala Mkristo hataishi kwa huo mzoga umeoza uliotoka kwa mafundisho ya kale ya kidhehebu na kadhalika. Wanataka Neno la Mungu lipya la siku hizi, ile ahadi ya wakati huu.

128 Mungu aliahidi sungura siku za Luther. Akaahidi vitu vingine katika siku za wengineo. Bali sasa ameahidi orodha kamilifu ya chakula, zile sehemu saba za orodha ya vyakula, kwa maana Mihuri zote Saba zimefunguliwa na kila kitu ki

tayari kwa ajili ya Neno la Mungu, kwa wale ambao wanaweza kulipokea . . .

129 Kengewa wanaorukaruka kama mwewe. Jamani! Waza hayo, jinsi ulivyo wa hatari nini—jinsi wakati huu ulivyo. Kama tu vile kengewa amepoteza thibitisho lake kama kengewe kwa muda mrefu, vivyo hivyo kanisa nalo limepoteza kwa muda mrefu thibitisho lake kama ndege ndugu mdogo wa tai, manabii wa Mungu. Zamani lilikuwa chukuzi la neno la kweli, kuhesabiwa haki, ndipo likawa chukuzi la kutakaswa, ndipo likawa chukuzi la ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudishwa kwa zile karama. Bali linapoendelea na kuzidi kurudi nyuma likijaribu kula vitu fulani, mana ya siku zingine, iliyooza. Haifai kitu. Tai halisi wa siku hizi anajua hiyo ilikuwa kweli, bali tuna hayo na mengine zaidi hata Yesu Kristo amedhihirishwa katika utimilifu wa uweza Wake kama alivyoahidi ingekuwa katika siku hizi za mwisho.

130 Sasa limekuwa kapi lililokauka. Limekwisha. Roho wa Mungu amepita na kuondoka kwake. Ni kweli. Nalo halita—halitarithi pamoja na mbegu Neno lililothibitishwa. Halitarithi kabisa. Halitanyakuliwa. Litakuwa mfuasi wa kanisa, labda lifufuke katika ufufuo wa pili, likahukumiwe kulingana na yale lililosikia. Iwapo uko hapa usiku wa leo kama tu mfuasi wa Kanisa hukumu yako itakuwaje sote tutakaposimama pale na kushuhudia ya kwamba ulisikia ukweli? Unaona?

Haruki tena angani, kuingilia yasiyojulikana, hata kwenye ya kimbinguni ambapo uweza, na vimo katika ahadi za Neno la milele la Mungu limefanya mambo yote kuwezekana kwa hao waaminio. Halitaamini hayo. Linasema . . . Litarudi nyuma kwenye waya za simu na kusema, "Dhahebu langu linasema ya kwamba sungura wametosha." Ingawa wana mabuu, ni wazuri haidhuru. Mnaona? Linategemea hayo.

131 Pentekoste sasa ni kama wale dada zao mwewe wa kidhehebu wanaoketi sasa kwenye viti vikubwa vya mabaraza ya wasio haki (bila shaka!), wakisikiza kiongozi wao mwenye siasa za kilimwengu, akiwalisha kwa chakula cha mwewe cha sungura waliokufa wa jambo lililopita miaka hamsini iliyopita. Hiyo ndiyo hali ya kanisa la Pentekoste. Jamani!

132 Kama vile Sara alivyojaribu kutimiza ile ahadi ya mambo ya kimbinguni kwa, kwa kujichagulia mwenyewe Hagai, vivyo hivyo kanisa linajaribu kuleta ufufuo, waijilisti wetu mashuhuri, kote nchini siku hizi, "Ufufuo katika wakati wetu, ufufuo katika wakati wetu. Ninyi nyote Methodisti, Wabaptisti, Pentekoste, nyote unganeni." Mwawezaje kupata ufufuo wa mana mpya kwa mzee mwewe wa kale aliyekufa?" Mwawezaje kupata? "Ufufuo wakati wetu." Ufufuo ungekuwa mdogo sana, hawangalijua kamwe ukitendeka.

133 Wapentekoste walisema, "Naam, jambo kuu litatendeka" Linatendeka, nao hawajui. Hiyo ni kweli. Mwaona? Naam, bwana! "Kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai . . .?. . ." Hivyo ndivyo ilivyosema. Je, mzoga ni nini? Neno. Yeye ni Neno, mzoga, Kristo, Kristo ndani yako, yeye yule jana leo, na hata milele.

134 Jinsi ilivyo kweli, Sara akijaribu kufanya ahadi yote itimizwe (mnaona?), katika ka—kanisa kuu kama la siku hizi, ufufuo mkuu wakati wetu kwa jinsi gani? Kwa ahadi iliyopotoshwa. Mtaufanyaje na huku Mungu hajabariki dhehebu kamwe? Yeye hakutumia dhehebu kamwe. Ujumbe ulipotangazwa, nao wakaunda dhehebu, lilikufa papo hapo. Namhimiza mwanahistoria ye yote anionyeshe ambapo lilipoinuka tena. Lilikufa papo hapo na kubaki papo hapo. Mungu aliondoka moja kwa moja kutoka chukuzi hilo akaingia kwenye lingine, katoka moja kwa moja kwa Walutheri akaingia katika Wamethodisti, mara katoka kwenye Wamethodisti kaingia kwenye Wapentekoste.

135 Sasa, Yeye ameondoka kwa Wapentekoste akaingia kwenye ile Mbegu, kwa maana haina budi kuwa Mbegu. Hauwezi ukashinda maumbile. Halingefanyika kingine ila kuwa Mbegu. Kwa hivyo ile Mbegu itajizaa Yenyewe, ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Nguzo ile ile ya Moto, ikionyesha ishara zile zile, uweza ule ule, Mungu yule yule, ishara zile zile, mambo yale yale. Amethibitisha Neno na Biblia vile vile, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye anaongoza usiku wa leo. Mungu atusaidie kuona hayo na kuamini. Hakika!

136 Mnaona Sara, kanisa, likijichagulia Hagai. Haikufaulu, sivyo? La! Wala kundi lake alilojichagulia halitafaulu leo pia. Madaktari, na ma Ph.D, na ma L.L.D. hayafai kitu. Chukuzi zote hazifaulu. Luther alishindwa; Hagai alishindwa. Hagai alifanyaje? Hagai alimtoa mwanawe akamweka kifuani mwa mwanamke mwingine (sivyo?) kumlelea mwanawe. Hagai alifanya hivyo, akamtoa mwanawe, mwanawe wa pekee, kifuani mwa mwanamke mwigine, asiye mama yake, kumlea. Ndivyo hasa Luther alivyotenda, alipomtoa mwanawe kuhesabiwa haki kwa dhehebu kumchezea (ndivyo hasa!), lipate kumlea.

137 Wesley alishindwa jinsi Sara alivyoshindwa, akitilia shaka kule kuzaliwa kimbinguni kuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, jinsi Sara alivyofanya kwenye ule mwaloni. Wesley alipojulishwa ya kimbinguni . . . Wakati wa Kipentekoste ulipoanza na Wesley akajulishwa kunena kwa lugha, haya yote, walilichekelea na kulifanyia mzaha. Ninyi nyote wa Church of Christ, nanyi (mnaojiita)—enyi Wabatisti, na Wapresbeteria, kila mmoja wenu aliuinulia pua lake na kuuondokea. Hiyo ni kweli! Ulifanyaje ewe Wesley? Uliuza mwanao kwa dhehebu, naye akafa na akaangamia. Hiyo ni kweli hasa.

138 Bali lile Neno, Neno la kweli likasonga mbele moja kwa moja. Halikukaa kwenye dhehebu hilo. Lilisonga mbele hata likaingia Pentekoste na kuchukua wengine zaidi pamoja nalo. Likawa mwana aliyekomaa zaidi, kama ile mbegu iliyoangukia kwenye tumbo la uzazi. Muda si muda likaanza kwenye uti wa mgongo, ndipo mapafu, na likapata kichwa pamoja na miguu, na muda si muda likafikia ambapo lilipozaliwa. Naam! Kwa hivyo hivyo ndivyo kanisa limekomaa, njia ile ile.

139 Wesley alitilia shaka jinsi hasa Sara alivyofanya kule mtini. Yeye alisema...Wakati malaika wa Bwana, Mtu aliyevalia kama ma—malaika . . . Mungu, alikuwa Yeye Mwenyewe, Elohim, aliyevalia kama mwanadamu aliyesimama pale na vumbi nguoni Mwake na kusema kwamba angefanya hivyo na akampa ahadi, baada ya Sara kuwa na umri wa miaka tisini na Ibrahimu miaka mia moja. Naye Sara akacheka moyoni mwake, na kusema, "Hii ingewezekanaje mimi na Ibrahimu hatujakuwa, vema, hatujakuwa kama vijana—uhusiano wa jamaa—labda kwa miaka ishirini." Alikuwa na karibu umri wa miaka mia moja. Kasema, "Mimi, mimi nipate furaha na bwana wangu, niwapo mkongwe na yeye mkongwe pia? Na mbegu zake za uhai zimekufa, na tumbo langu la uzazi limekauka. Sina matiti, mishipa ya maziwa imekwisha. Ningeipataje?" Mungu akasema, "Niliahidi. Atakuja kwa kila hali."

140 Vivyo hivyo Wesley. "Tunawezaje kukubali huko kunena kwa lugha, na uponyaji wa Kiungu, na upuzi. Si kwa ajili yetu siku hizi."

141 Mungu akasema, "Mimi niliahidi katika siku za mwisho ya kwamba nitawamwagia watu wote Roho yangu." Yeye aliahidi kufanya hivyo, na akafanya hivyo kwa vyo vyote. Nalo kanisa la Kiwesley pamoja na—maskini dada zake mbelewele wa Kibatisti, Presbeteria, na Church of Christ, na Nazarenes, Pilgrim Holiness, na United Brethren, na kadhalika wakafa moja kwa moja pamoja nalo, nalo Kanisa likasonga mbele. Sasa, Pentekoste walifanyaje? Wakaunda dhehebu kama tu lile Kapi. Lilifanya jambo lile lile. Likaungana pamoja, likajifanya kama lile kapi. Hiyo ni kweli!

142 Petekoste ilikuwa Mariamu. Karamu ya Pentekoste, tazama aliyotenda Mariamu. Mariamu alikosea wapi? Kwenye karamu ya Pentekoste wakati mmoja alikabiliwa na kundi la watu mashuhuri, makuhani wakati mwanawe...Hangempata po pote. Naye akarudi nyuma safari ya siku tatu. Alikuwa amemwacha kama kanisa la kisasa siku hizi, kanisa limemwacha kwa muda wa karibu miaka mitatu mara tano ama ishirini na mitano wamemwacha—kadiri ya miaka hamsini iliyopita ama sabini na mitano.

143 Alimwacha kwenye karamu ya Pentekoste. Mariamu akarudi nyuma pamoja na Yusufu siku tatu wakimtafuta. Alikuwa

akimtafuta, asimpate. Alimpata. Alipata nini? Alimpata hekaluni akihojiana juu ya Neno la Mungu na makuhani. Na papo hapo mbele ya makuhani hao, hao watu mashuhuri, Mariamu akashusha pazia. Alifanya hasa jambo ambalo haikumpasa kufanya. Mwamwita yeye Mungu—mama wa Mungu? Inampasa mama kuwa na hekima kuliko mwanawe. Naye akasema, "Baba yako na mimi tumekutafuta kwa huzuni usiku na mchana. Baba yako na mimi . . . " Akidai ya kwamba kuzaliwa Kwake hakukuwa kwa kimbinguni, ya kwamba Yusufu ndiye baba wa Yesu. Akakana ule uzazi wa kimbinguni. Pentekoste ilichukua kunena kwa lugha. Wakakana uzazi wa Neno. Hivyo ndivyo walivyofanya hasa. Watachukua sehemu fulani yake, bali hawatachukua kila kitu. Ilikataa ule uzazi wa Neno jinsi tu Mariamu alivyofanya.

144 Bali tazama, hakutakuweko na madhehebu mengine baada ya hili. Tazama! Neno Lenyewe—walakini umri wa miaka kumi na miwili, kitu kidogo tu kule nyuma kwenye kapi—Yeye akasema, "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika kazi ya Baba Yangu?" Neno likalisahihisha kanisa papo hapo.

145 "Je, ya nini mambo haya yote unayofanya? Unajua huwezi kufanya hivi. Tutakufungia milago yetu. Hatutakuruhusu kuingia."

146 "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika kazi ya Baba Yangu?" Naam, naam, uzuri halisi wa kimbinguni.

147 Yeye alidai ya kwamba Yeye ni mwana wa Yusufu tu, mtu tu, ama jinsi walivyotenda Wapentekoste, wakadai kuwa Yeye ni mmoja wa wale watatu (whiuu, najua hili linawaudhi!)—mmoja wa wale watatu, bali alikuwa wote watatu katika mmoja. Bali Wapentekoste, "Oh, naam, Yeye ni Mwana wa Baba na Roho Mtakatifu . . . " Jamani! Bali Yule Neno halisi na wa kweli hunena waziwazi na kusema, "Hao si watatu; ni mmoja." Hamjui Neno la Mungu. Inawafanya, si watatu, bali mmoja.

148 Tazama, hapatakuweko chukuzi jingine, makanisa mama, madhehebu, baada ya kapi hili bebaji kwa maana baada ya kapi hamna tena . . . Hamna kilichosalia tena, bali punje tu. Sivyo? Huenda kwenye punje. Haina budi kuwa aina ile ile iliyopandwa, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

149 Roho yuaja juu ya Bibi-Arusi kufanya mambo yale aliyofanya. Mnaona, ni kujizaa tena kwa ile punje.

150 Lile Neno, ijapokuwa lilikuwa changa, likajitetea! "Na hamjui ya kwamba imenipasa kuwa katika kazi ya Baba Yangu?"

151 Hiyo ndiyo siri ya Ujumbe sasa. Hiyo hasa, kazi ya Baba, Je, kazi ya Baba ni nini? Je, waweza kuwaza kazi ya Baba ilikuwa nini Kwake? Kutimiza aliyosema Isaya, "Bikira atachukua mimba." Kutimiza aliyosema Isaya tena, "Mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu," na mambo haya yote

ambayo yangetendeka; kama alivyosema Musa, “Bwana Mungu atawaondokeshea nabii miongoni mwenu mfano wangu mimi.” Ilikuwa kazi ya Baba Yake kutimiza Neno hilo. Vema, ikiwa lilipitia kwa ubua hizi za wanawake hawa wa kawaida, je na ubua hizi za makanisa wanawake wa rohoni? Makanisa maana yake ni wanawake—wanawake maana yake ni makanisa, hasa. Sivyo? Basi ni nini sasa? “Inatupasa kuwa katika kazi ya Baba!” ngano itapasa sauti tena, ile punje. Naam, bwana! Inapaswa kufanya nini? Kuthibitisha Malaki 4; ithibitishe Luka 17:30; ithibitishe Waebrania 13:8; ithibitishe Yohana Mt 14:12; ithibitishe Neno Lake lote: ithibitishe Waebrania—nanamaanisha—Ufunuo sura ya 10; ya kule kufunguliwa kwa zile Mihuri Saba; na zile siri za Mungu, hata kufikia uzao wa nyoka, na yote yangedhihirishwa: Ndoa na Talaka na siri hizi zingine zote ambazo zimefichwa chini ya zile nguzo tangu miaka hii yote kutoka kwa wanatheologia na kadhalika, bali sasa ni wakati wake. Hiyo ndiyo kazi ya Baba. Wafikiri wao wataipokea? Wanataka kujifanya waungwana na kusema, “Dhehebu letu halitufundishi hayo!” Bali Biblia inawafundisha! Naam! Mungu huithibitisha kuwa kweli. Bila shaka.

152 Ikitimiliza wakati huu ambapo zile Mihuri Saba tayari zinathibitisha kwamba madhehebu yamekuwa tu wachukuzi. Hiyo ni kazi nyingine ya baba. Kuthibitisha. . . Na kazi ya Baba sasa ni kuwaonyesheni ninyi haya madhehebu si Yake. Ni mipingo iliyobuniwa na binadamu ambayo hukana Neno. Naam!

153 Tazama! Mnasema, “Kwani, Mariamu yule—yule Bikira mkuu?” Msalabani Yeye hakumwita, “mama,” alimwita, “mwanamke,” mchukuzi, si mama. Kweli, alikuwa mchukuzi wa lile Neno, bali hakuwa Neno. Yeye ndiye Neno. Naam!

154 Tazama pia, Mariamu hakushirikishwa katika ufufuo pamoja Naye. Yeye alikufa na akafufuka tena, maana alikuwa Neno. Mariamu alikuwa tu mchukuzi. Alikufa na yungali kaburini. Hiyo ni kweli! Kwa hivyo alikuwa mchukuzi tu, si mama Yake, si Mungu. Alikuwa tu mchukuzi jinsi makanisa yalivyo. Kweli hasa! Inaonyesha alikuwa mchukuzi tu, si Neno.

155 Hebu tumalizie kwa kusema hili. Jamani, enyi kengewa wa Kipentekoste, mnaoruka-ruka kama mwewe, mkishiriki ya ulimwengu jinsi tu wengine wafanyavyo, mlio na mfano wa utauwa, wa kutosha mpate kuwapoteza walio Wateule kama yamkini, lakini mkikana nguvu zake, kama asemavyo nabii hapa, mfano mkamilifu wa jinsi Neno la Mungu lilisema ingekuwa katika siku za mwisho, wakati wa kanisa Laodikia, uchi, kipofu, lenye mashaka, maskini, nyonge na halijui likidai ya kwamba ni kubwa na tajiri, halina haja na kitu, na halijui ya kwamba limebadilika kutoka kengewa, ndugu aliyefanana na nabii apate kulainisha Neno la Mungu, likawa mwewe na linawalisha watu wake kwa sungura wa kidini waliokufa. Bila

shaka, hasa! Amkeni! Jamani, mnatumainiaje kushirikishwa—au kurithi pamoja na tai mkiwa na mambo kama hayo katika saa hii iliyo kuu ambapo kunyakuliwa kumewadia.

156 Ee, Mkristo, ee, muumini, iwapo umekuwa muumini nusu, endelea kuhudhuria mikutano kwa muda kidogo tu, utafanya hivyo? Tuna jambo hapa ambalo naamini Bwana anataka mjue. Imechelewa; siwezi kuendelea zaidi. Sina budi kukoma, na labda nitamaliza kesho usiku. Bali tazama, na tuinanishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

157 Siwataki muone ufasaha wangu wa lugha ninayotumia, bali nawatakeni myashike kwa dhati kwa kitambo kidogo yale niliyosema. Ni dhahiri kutosha hata mngeweza kufahamu, nina hakika, mkitaka. Iwapo uko hapa usiku wa leo, nawe huna ujuzi huu. . . Sisemi. . . Unasema, "Nimecheza katika Roho, nikaruka-ruka kila mahali." Naam, kengewa hufanya vivyo hivyo. Ni kama kunguru na Mwewe. Si ulizi hilo. Je, unakula nini? Je, unapata wapi mlo wake wa kila siku? Unakula kutoka wapi, kwa Neno la Mungu ama nyama zilizooza zilizotumiwa kule nyuma miaka kadha wa kadha iliopita? Je, ujuzi wako hata usiku wa leo ni wa kitu ulichookota miaka mingi iliyopita, au ni wa kisasa na mpya usiku wa leo, mana mpya ambayo imeanguka hivi sasa tu kutoka mbinguni na unalisha nafsi yako kwayo na kutazamia kupata jambo nzuri na bora zaidi kesho? Kama sivyo ulivyo, sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na macho yenu yamefungwa, na mioyo yenu imeinamishwa, jiulize swali hili aminifu—na si kwangu bali kwa Mungu—ungeweza kuinua mkono wako kwa ushuhuda ukisema hivi? Mungu; andaa nafsi yangu na roho yangu nipate kujilisha kwa Neno la Mungu pekee. Je, waweza kuinua mkono wako, useme. . . Mungu akubariki! Mungu akubariki!

158 Sijui ni wangapi hasa waliomo humu ndani, kuna—usiku wa leo. Sijui kupima wingi wa watu; bali ningesema yapata theluthi moja au zaidi waliinua mikono yao, ya kwamba wanataka nafsi zao ziandaliwe. Na tukumbuke katika maombi tunapoinamisha vichwa vyetu.

159 Mungu mpendwa, kazi yangu nikusema tu Neno. Na kwa mafumbo madogo haya na rahisi, mifano midogo, watu wanaona ya kwamba mmoja hatarithi na mwingine. Na tunajua ya kwamba katika siku za mwisho kutakuweko watu ambao watakaonyakuliwa mbinguni. Na wengine wao watakuwa hapa Yesu ajapo. Nasi tunamtazamia aje hata usiku wa leo.

160 Nami nafikiri yapata kama miaka thelathini ama thelathini na mitatu iliyopita nilipiga magoti labda saa kama hizi za usiku, kama saa 3:30 au saa 4:00, nikimwombea baba aliyekuwa mpotevu. . . Usiku wa leo, Bwana, nawaombea baba wengi, mama wengi, na ndugu, na dada. Si uwahurumie, Mungu mpendwa? Imechelewa sana kwa baba yangu kufanya cho chote

kuhusu haya; tayari amekwisha kupita ng'ambo ya mipaka ya maisha haya. Na hivi karibuni, Bwana, sote tutapitia njia hiyo. Mimi pia sina budi kupitia njia hiyo. Kila mwanamume na mwamamke, kijana ama msichana humu ndani hana budi kupitia hiyo njia. Nasi tutajibu vile tumetenda na Neno la Mungu.

161 Jinsi huyo mtu alivyoonekana duni sana mbele ya Daudi alipokuwa anamtemea mate. Jinsi watu hao watakavyofikiria machache ambao walimtemea mate Yesu aliye Neno, atakaporudi tena, wale waliomchoma. Jinsi watu hao watajiona duni sana ambao wanaweza kuondoka hapa na kuona hata si katika maneno makuu ya Kiyunani na kadhalika bali katika maumbile laini ambayo yanafundisha juu ya Mungu aliye Muumba—wanaweza kuona chukuzi za Neno, na kuona Neno lenyewe, na kujua saa tunayoishi, na ya kwamba wakati wa mavuno umewadia. Mungu mpendwa, hebu na tusiyape kisogo kwa ajili ya upuzi wa ulimwengu, bali hebu na tumpokee Yeye usiku wa leo kwa mioyo yetu yote.

162 Nawe Bwana, kaumbe ndani yangu roho zuri, Roho ya Uzima, nipate kuamini maneno Yako yote na kumkubali Yesu, aliye Neno, yeye yule jana, leo, na hata milele, na nikaamini leo ile sehemu ambayo imekusudiwa kwa wakati huu. Tujalie, Bwana. Naomba katika Jina la Yesu.

163 Na sasa nitamuulizeni kila mmoja wenu mlio hapa mnapowaza haya kwa moyo mweupe sana. . . Hatuna kanisa mgalijiunga nalo. Tuna kidimbwi pale cha kubatiziwa: "Nao walioamini wakabatizwa." Iwapo hujabatizwa bado katika ubatizo wa Kikristo. . . Hiyo haimaanishi kunyunyiziwa, kumwagiwa maji; maana yake ni kwa kuzikwa, si katika cheo cha Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, bali katika Jina la Yesu Kristo jinsi kanisa nzima lilivyobatizwa hadi kanisa Katoliki katika mwaka wa 303 lilipoingiza miungu mitatu na namna tatu za ubatizo katika utatu wa vyeo. Iwapo hujapata huo bado, kesho asubuhi saa 4:00, kuna majoho na kadhalika yanayokungoja kule chini.

164 Si uje ukajiunge na Yesu Kristo, si pamoja nasi. Hatuna kanisa hata hapa kukuhudumia. Nenda kwa kanisa lo lote utakalo, po pote unapotoka, bali nakusihi, amini Neno hili. Je, mnaliamini, semeni "Amina!" [Makutano wanajubu, "Amina! "—Mh.] Mungu awabariki! Na mfanye. . .

165 Iwapo mna jambo tunaloweza kuwaasaidia, tuko hapa kufanya hivyo.

166 Sasa, najua kuna wagonjwa hapa. Wakati umetuishia wa kufanya mstari wa maombi. Labda tutaupata hata hivyo. Nataka kila mmoja wenu anifanyie jambo fulani. Umeketi karibu na mtu fulani, wekelea mikono yako juu ya mtu huyo. Na bila shaka umeweka mikono yako juu ya tai,

labda tai ambaye amekuwa akila chakula cha mwewe mahali fulani, kikamchosha. Hawakitaki tena. Wanataka kukiacha. Wamekikinai na kimewachosha. Kaketi hapa usiku wa leo na kuona kile tai wanaweza kula, Neno, na kuwa na Kristo aishiye akiishi miongoni mwao, akijionyesha kuwa yu hai, yeye yule leo, jana, na hata milele. Hawataki kurithi pamoja na makapi. Hayo yatachomwa moto. Majani makavu yote na kadhalika yatachomwa moto. Kile chombo cha kuvunia kinakuja kutwanga ngano. Unataka kuwa ngano.

167 Kuna wengine wao walio wagonjwa, baadhi yao wagonjwa kimwili, nawatakeni muombe. Tai, mwombee ndugu yako, dada tai pale, ninapowaombeeni hapa. Roho wa Mungu na aje juu yenu.

168 Kumbukeni, nawapeni chakula cha tai, ile ahadi ya Mungu. Yeye huwaita manabii wake tai. Yeye anajiita Tai, Yeye ni Yehova Tai. Na mnapowekeleana mikono yenu ninyi kwa ninyi, waombeeni.

169 Baba yetu uliye mbinguni, Neno Lako lilisema, agizo la mwisho ulilotoa kwa Kanisa Lako, lilikuwa. "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili—agizo kwa watu wote—aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya; wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wakishika nyoka, hawatawadhuru kamwe; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ee Yehova Tai, walishe watoto Wako usiku wa leo kwa hilo Neno, Bwana. Wao ni wahitaji. Huo ndio mlo wanaohitaji. Hicho ndicho wanachohitaji, kujua ni chakula gani, ni nini BWANA ASEMA HIVI.

170 Uliahidi kwamba kama wakiwekeana mikono wao kwa wao watapata afya. Ee Bwana, ondoa tashwishi yote na mawazo ya mwewe kutoka kwetu sasa. Nasi tujilishe kwa uchaji kile chakula cha Tai cha Neno la Mungu.

171 Na kila roho mchafu aliye ndani ya watu hawa, kila roho wa kufanya tashwishi, kila roho wa hofu, kila dai la kidhehebu, kila tabia, kila maradhi, kila ugonjwa ulio miongoni mwa watu na viondoke, katika Jina la Yesu Kristo na viondoke kwa kundi hili la watu. Na wawe huru tangu sasa na kuendelea, wapate kula kile Chakula cha Tai tunachoamini utatutumia juma hili lote, Bwana, kufungua zile Mihuri na kutuonyesha siri hizo zilizofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, kama ulivyoahidi. Wao ni Wako, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

172 Wote wanoamini na kukubali, simameni, mkasema, "Naamini, nakubali hayo; yale Mungu aliyoniahidia, nayapokea." Bwana awabariki. Hiyo ni ajabu. Kila mtu anasimama. Hilo ni zuri! Wimbo *Nampenda*. Na tumwimbie

Yeye wimbo huu basi, Nampenda, nampenda, kwani alinipenda kwanza . . . Wote pamoja sasa.

> Nampenda, (kama ndivyo, na tuinue mikono yetu!) Nampenda,
> Kwani alinipenda kwanza
> Na akanunua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

173 Lo, si ni wa ajabu? Na tuamkuane kwa mikono sisi kwa sisi. Ndugu Tai, geuka tu, dada, amkuana kwa mikono tunapoimba.

> Nampenda, . . .
> [Makutano waamkuana—Mh.]
> Mtini Kalvari.

Na tumwinulie mikono yetu tena.

> Nampenda, nampenda,
> Kwani alinipenda kwanza (Naye hutufanya sisi tai!)
> Na akanunua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

174 Utajuaje, walimwengu watajuaje ya kwamba unampenda Yesu? Tunapopendana sisi kwa sisi. Hivyo ndivyo walimwengu . . . Mnaona, Mungu anaona imani yenu, walimwengu wanaona matendo yenu, Pendaneni sasa; karimianeni. Zungumzeni ninyi kwa ninyi. Vumilianeni. Na mawaidha yo yote tunayoweza kuwapeni, ubatizo, kumtafuta Roho Mtakatifu . . . Hatuna nafasi hapa kufanyia hayo, mwafahamu. Mwito wa madhabahuni, iwapo Mungu alikuhakikishia kwamba hii ni kweli, ya kwamba Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, na unataka kuungana pamoja naye, nenda kabatizwe katika Jina Lake kesho. Kutakuweko watu kule watakaokushauri. Cho chote tunachoweza kufanya kukusaidia tutafanya.

> Nampenda, Nampenda
> Kwani (Ninyi mlio kwenye simu sasa, Tucson, kule California, kote mashariki, inueni mikono yenu kule kote . . . ? . . . Msifuni!)
> . . . kanunua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

175 Naam, hadi kesho usiku nawakabidhi kwa Ndugu Neville mchungaji wetu.

Ile Mbegu Haitarithi Pamoja Na Kapi SWA65-0218
(The Seed Is Not Heir With The Shuck)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, Februari 18, 1965, katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Ya Parkview Junior kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2014 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org